**HOTUBA YA IJUMAA**

KAZI HESHIMA**.**

**Imefasiriwa**

**na**

**Profesa.Ayman Alasar**

Shukrani njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe. Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake:

**وَقُلِ اعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ  وَسَتُرَدُّونَ إِلَى عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ.**

{**Na sema: Tendeni vitendo. Mwenyezi Mungu na Mtume wake pamoja na Waumini wataviona vitendo vyenu. Na mtarudishwa kwa Mwenye kujua siri na wazi; naye atakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda**}.

Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika. Na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wake na mja wake.

Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utagulizi huo**:

Dini ya Kiislamu imeliangalia swala la kufanya kazi kwa mtazamo mkubwa na kuitukuza, kwani kazi ndio njia ya ustawi na maendeleo, mwenye kuzingatia ndani ya Quran Tukufu atakuta wito wa wazi wa watu kutakiwa kufanya kazi ambayo hupelekea ujenzi wa ulimwengu, na kufikia mafanikio kwa dunia yote, ambapo Anasema Mola Mtukufu: **هُوَ أَنْشَأَكُم مِّنَ الأَرْضِ وَاسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا** {**Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo**}. Na Anasema Mola Mtukufu:

هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ ذَلُولًا فَامْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا مِنْ رِزْقِهِ وَإِلَيْهِ النُّشُور.

{**Yeye ndiye ambaye ameidhalilisha kwenu ardhi basi tembeeni kwenye pembe zake na mule katika riziki zake na kwake ndio marejeo**}. Na Anasema tena Mola Mtukufu: **فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِنْ فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيراً لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ**

{**Pindi mnapomaliza Ibada ya swala basi nendeni maeneo mbalimbali tafuteni fadhila za Mwenyezi Mungu, na mumtaje Mwenyezi Mungu kwa wingi ili mfaulu**}.

Umuhimu wa kufanya kazi umekuja moja kwa moja baada tu ya amri ya Ibada ya swala, na Iraki Ibn Maliki R.A alikuwa akishamaliza kuswali swala ya Ijumaa hutoka na kusimama kwenye mlango wa Msikiti akisema: Ewe Mola mimi nimeitikia wito wako na nimeswali swala yako, na nimetoka kama ulivyoniamrisha, hivyo naoma uniruzuku kutokana na fadhila zake na Wewe ni Mbora wa kutoa riziki.

Kama vile Sunna nyingi Takatifu za Mtume S.A.W zimetoa wito wa kufanya kazi kwa bidii kubwa, kwa kuzingatia kwake kazi hujenga heshima na kulinda hadhi ya na heshima ya mwanadamu, ambapo Mtume S.A.W anasema:

**أفضلُ الكسْبِ بيعٌ مبرورٌ، وعملُ الرجلِ بيدِه**

"*Pato bora ni biashara inayokubalika Kisharia, na kazi anayoifanya mtu kwa mikono yake*". Na anasema tena Mtume S.A.W:

**لأن يَحْتَطِبَ أَحَدُكُمْ حُزْمَةً عَلَى ظَهْرِهِ خَيْرٌ لَهُ مِنْ أَنْ يَسْأَلَ أَحَدًا فَيُعْطِيهِ أَوْ يَمْنَعُه.**

"*Mmoja wenu akifanya kazi ya kukata kuni kuzibeba na kuziuza ni bora kwake kuliko mmoja kufanya kazi ya kuomba akapewa au akanyimwa*". Na Sufyani At-Thaury R.A alikuwa anapita kati ya watu wakiwa wamekaa Msikitini wa Makka akiwauliza, ni kitu gani kimewakalisha humo, wakajibu: Tufanye nini? Akasema: Nendeni mukatafute fadhila za Mwenyezi Mungu wala musiwe watoto kwa Waislamu, na anasema Omar Ibn Khattab R.A asikaye mmoja akiomba riziki na

anasema: Ewe Mwenyezi Mungu niruzuku, wakati mumefahamu kuwa mbingu hainyeshelezi dhahabu wala fedha.

Kutokana na heshima ya kazi na umuhimu wake Manabii wa Mwenyezi Mungu *Amani ya Mola iwe kwao* walikuwa wanafanya kazi kwa mikono yao, ambapo Mtume wetu Muhammad S.A.W anasema: “Nabii Daudi *Amani iwe kwake* alikuwa anakula kwa kazi za mikono yake” na anasema pia: “Nabii Zakaria *Amani ya Mungu iwe kwake* alikuwa fundi seremala” na Mtume mwenyewe S.A.W alikuwa anafanya kazi mwenyewe, na alikuwa akifanya kazi za kusaidia familia yake, anasema Bibi Aisha Radhi za Mungu ziwe kwake: Mtume S.A.W alikuwa akishona viatu vyake pamoja na nguo zake, kama vile Mtume S.A.W ametulingania kufanya kazi mpaka dakika ya mwisho ya maisha yetu, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W:

**إِنْ قَامَتِ السَّاعَةُ وَبِيَدِ أَحَدِكُمْ فَسِيلَةٌ ، فَإِنْ اسْتَطَاعَ أَنْ لاَ يَقُومَ حَتَّى يَغْرِسَهَا فَلْيَفْعَل .**

“*Kitakapo simama kiyama na mkononi mwa mmoja wenu akawa na mche wa mti, basi ikiwa ataweza kuupanda kabla ya kiyama akijasimama basi na afanye hivyo*”.

Kutokana na heshima ya kazi Sharia ya Kiislamu imefanya kwa kila mwenye kufanya kazi kwa ajili ya maisha yake na riziki za watoto wake ana malipo ya shahidi, kwani Quran Tukufu imeunganisha kati ya kazi na kujitoa muhanga katika njia ya haki, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

**وَآخَرُونَ يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ يَبْتَغُونَ مِن فَضْلِ اللَّهِ وَآخَرُونَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ.**

{**Na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta fadhila za Mwenyezi Mungu, na wengine wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu**}, pindi mtu mmoja alipopita kwa Mtume S.A.W Maswahaba wa Mtume S.A.W wakamuona yule mtu kutokana na nguvu zake na uchangamfu wake kitu kilichowashangaza wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu lau huyu mtu angekuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu! Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W.

إِنْ كَانَ يَسْعَى عَلَى وَلَدِهِ صِغَارًا فَهُوَ فِي سَبِيلِ اللهِ، وَإِنْ كَانَ خَرَجَ يَسْعَى عَلَى أَبَوَيْنِ شَيْخَيْنِ كَبِيرَيْنِ فَفِي سَبِيلِ اللهِ، وَإِنْ كَانَ خَرَجَ يَسْعَى عَلَى نَفْسِهِ لِيَعِفَّهَا فَفِي سَبِيلِ اللهِ، وَإِنْ كَانَ خَرَجَ يَسْعَى عَلَى أَهْلِهِ فَفِي سَبِيلِ اللهِ.

"*Ikiwa atafanya kazi kwa ajili ya watoto wake wadogo basi anakuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, anapotoka kwa ajili ya kuhudumia wazazi wake wazee anakuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, ikiwa anatoka kwa ajili ya nafsi yake ili kujitosheleza mahitaji yake anakuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, na ikiwa anatoka kwa ajili ya familia yake basi anakuwa katika njia ya Mwenyezi Mungu*".

*******

**HOTUBA YA PILI**.

Shukrani zote za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, rehma na amani zimwendee mbora wa viumbe naye ni Mtume wetu Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Uislamu haujatutaka sisi kufanya kazi tu bali umetuhimiza juhudi na umakini wa kazi ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuahidi kwa mwenye kufanya kazi kwa umakini mkubwa kumpa malipo kwa maana ya thawabu nyingi, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا.

{**Hakika wale walio amini na wakatenda mema – hakika Sisi hatupotezi malipo ya anaye tenda mema**} kama vile kufanya kazi kwa umakini ni katika mambo ambayo Mwenyezi Mungu anayapenda ambapo anasema Mtume wetu S.A.W:

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ إِذَا عَمِلَ أَحَدُكُمْ عَمَلا أَنْ يُتْقِنَهُ.

“*Hakika Mwenyezi Mungu anapenda pindi mmoja wenu anapofanya kazi kuifanya kwa umakini*”.

Uaminifu wa kazi ni jukumu lipo shingano mwa kila mfanya kazi anaangaliwa na Mola wake Mtukufu, ambapo anasema Mwenyezi Mungu: **إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا** {**Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalia**}. Na anasema Mola Mtukufu:

**وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلا فِي السَّمَاءِ وَلا أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ.**

{**Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yeyote katika Quran, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi**}. Na pindi alipoulizwa Mtume S.A.W kuhusu maana ya wema akasema: **الإِحْسَانُ أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ .**

“*Wema ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba unamuona, ikiwa wewe humuoni basi Yeye anakuona*”. Amesema kweli Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani ziwe kwake.

Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba utuwezesha kufanya mambo ya kheiri na uhifadhi Misri yetu na kila ubaya pamoja na kuzihafadhi nchi za ulimwengu wa Kiarabu na Kiislamu.

**Allahumma Amin.**